Toleo 68 - Safar 1444 H / Septemba 2022 M

# UQAB

Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Marekani haina Mamlaka ya Kimaadili Kulazimisha Rafiki au Adui kwa Afrika

**HABARI NA MAONI**
Uislamu na Waislamu Wataendelea Kuteseka Bila kujali Nani Ameshinda au Ameshindwa

**MATOLEO**
Je, Haiba ya Kimataifa Inapatikana kupitia Kuwatumikia Maadui wa Uislamu?

**JIBU LA SWALI**
Swadaqa Ya Mwana Mwema Kumtolea Mzazi Wake Aliyekufa, Thawabu Zitamfikia?

# CHAGUZI ZA KIDEMOKRASIA: HADAA INAYORUDIWA RUDIWA KWA UMMAH



Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسۡتَخۡلِفَنَّهُمۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ كَمَا ٱسۡتَخۡلَفَ
ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمۡ دِينَهُمُ ٱلَّذِي ٱرۡتَضَىٰ لَهُمۡ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعۡدِ خَوۡفِهِمۡ أَمۡنٗاۚ
يَعۡبُدُونَنِي لَا يُشۡرِكُونَ بِي شَيۡـٔٗاۚ وَمَن كَفَرَ بَعۡدَ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡفَٰسِقُونَ﴾

KUMB: 01/1444 | Alhamisi, 20 Muharram 1444 H | 18/08/2022 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Chaguzi za Kidemokrasia: Hadaa Inayorudiwa rudiwa kwa Ummah

Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka nchini Kenya (IEBC) imemtangaza naibu wa Rais William Samoei Ruto kuwa Rais mteule katika uchaguzi uliomalizika hivi punde. Muda mfupi kabla ya tangazo hilo, makamishna wanne wa IEBC walikanusha matokeo ya Urais kwa kusema; "yalifikishwa kwa njia isiyo wazi". Raila Odinda, mshindani mkuu wa Ruto katika uchaguzi huo, alikataa matokeo na kuapa kwenda Mahakama ya Upeo juu ya kushindwa uchaguzi. Ukisifiwa na waangalizi wa kimataifa kuwa kwa kiwango kikubwa ulikuwa wa amani na "juu ya wastani", uchaguzi huo ulikuwa na idadi ndogo kabisa ya wapigakura waliojitokeza katika kipindi cha miaka 15 huku wengi ya vijana wakisusia upigaji kura.

Sisi katika Hizb ut Tahrir Kenya tungependa kusema yafuatayo:

Chaguzi za Kidemokrasia huwa ni mbinu tu za kimpito kuondoa utawala mmoja na kwa kuuleta mwengine kwa maana huhalalisha utawala ufuatao. Mchakato huu kwa hakika hauakisi wala kuonesha uhakika wa zoezi la upigaji kura kama kigezo msingi bali huwa ni kupeana uhalalishaji tu wa uongozi mpya. Kwa hivyo, zoezi zima la uchaguzi ni sura ya kidanganyifu ya kidemokrasia na ukweli kuwa uteuzi badala ya uchaguzi. Fauka ya haya misemo ya ‘Uchaguzi huru, haki na wa uwazi' ni turufu tu ya Wakoloni Magharibi ili kutunga udanganyifu unaoweka kikomo mabadiliko ya uchaguzi na ratiba inayoitwa vikomo vya muhula.

Kuhusiana na suala la ususiaji wa wapiga kura, hii inaonesha bayana kwamba raia wengi na hasa vijana wamekosa imani kwa uongozi ambao kwa muda mrefu wameshindwa kutatua matatizo yao sugu. Raia wametambua kwamba viongozi wa kisiasa wana ubinafsi wa kisiasa ambao ndio kipaumbele kwao na nambari moja kuliko maslahi ya raia. Kiasili na kimaumbile mfumo wa Kibepari husababisha unyama wa kisiasa na uchu wa kupapia mali hivyo kuwanyima raia wa kawaida mahitaji msingi.

Tunaeleza bayana kwamba mfumo batili wa Kirasilimali ndio kiini kikubwa cha matatizo yote Kenya inayokumbana nayo miongoni mwake ni ubabe wa kutojali kwa wanasiasa, ufisadi uliozagaa, mfumko wa bei na utovu wa usalama. Matatizo haya sio kwa Kenya tu bali ni kwa ulimwengu kwa ujumla. Ubepari umejikita katika kuwatajirisha matajiri na kuwanyonya maskini hatimaye kusababisha pengo kubwa kati ya matajiri na maskini. Tuna hakika kwamba katika uchaguzi wowote wa kidemokrasia katika kipindi na wakati wowote hautawahi kutoa uongozi unaodhihirisha uimarikaji wa kweli badala ya uongozi unaofanya kazi kwenye mduara wa ushawishi wa dola za kibepari za kikoloni.

Kenya na dunia nzima inauhitaji pakubwa Uislamu na mfumo wake wa utawala (Khilafah) ulio na suluhisho la wazi la matatizo yanayowakabili wanadamu wote. Uislamu unaifafanua siasa kuwa ni kujali kwa dhati mahitaji ya watu na wala sio kuwania madaraka miongoni mwa wanasiasa wanaopigania manufaa yao binafsi. Mfumo ambapo dori ya vyama vya kisiasa haitakuwa kama vyombo dhidi ya maslahi ya Ummah. Badala yake vitapewa dori ya uangalizi ili kuhakikisha uongozi unatimiza wajibu wake na kuwafikishia raia wake wote.


**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari**
**Hizb ut-Tahrir Kenya.**

Afisi ya Habari
ya Hizb ut Tahrir
Tanzania

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

HIZB UT TAHRIR

KUMB: 01/1444 Jumapili, 01 Saffar 1444 H 28/08/2022 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Marekani haina Mamlaka ya Kimaadili Kulazimisha Rafiki au Adui kwa Afrika

Marekani inalazimisha kwa Bara la Afrika sheria yake ya kikoloni na ya kinafiki katika jaribio lake la kujeruhi athari ya Urusi, kuitenga na kuidhoofisha kufuatia uvamizi wake nchini Ukraine.

Marekani kwa kupitia ‘Sheria ya Kupambana na Matendo Maovu ya Urusi barani Afrika iliyopitishwa na Baraza lao la Wawakilishi, inaitaka Afrika kusitisha kujihusisha na Urusi ili kuhakikisha vikwazo vyake (dhidi ya Urusi) vinatekelezwa ndani ya bara hilo.

Kwa Sheria hiyo tajika ya Marekani inaelekeza na kulilazimisha bara la Afrika kwa kupitia Waziri wake wa Kigeni libainishe wazi wale wote wanaojihusisha na matendo ya Urusi barani Afrika, ambapo Marekani italazimika kuwaadhibu washirika hao (wa Urusi) kwa namna ambayo Marekani itaona inafaa, ikiwemo kuwawekea vikwazo au adhabu nyengine yoyote itakayoamuliwa na dola ya Marekani.

Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika imepinga hatua hizi za Marekani katika Mkutano wa karibuni wa 42 katika kikao chao cha kawaida cha wakuu wa nchi zao kilichofanyika jijini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambapo mkutano huo kwa pamoja walitoa msimamo kupitia waraka wao uliokataa rasmi, kuonesha kutoridhishwa kwao na kutokubaliana na sheria hiyo ya Marekani dhidi ya Urusi, wakiitaja sheria hiyo kuwa sio ya haki inayoilenga Afrika kwa hatua za kuidhabu kwa matakwa ya Marekani pekee.

Ni jambo la aibu ya wazi na unafiki usio na shaka kwa Marekani inayojizatiti kuinyoshea kidole Urusi na kuipaka matope kwa uvamizi wake nchini Ukraine, ilhali dola hiyo ya Marekani ikijisahaulisha uvamizi na ukaliaji wake wa kimabavu nchini Iraq, Afghanistan na nchi nyingine, wakiuwa kwa maelfu na kupora kusikokuwa na mfano. Pia Marekani daima imekuwa kimya kwa uvamizi wa Urusi na mauwaji yake kwa Waislamu wa Syria, kwa sababu tu jambo hilo liko sambamba na sera yake dhidi ya Uislamu wa kimfumo na kuuwa Waislamu.

Ukweli wa mambo si Marekani wala Urusi wana urafiki (wa kweli) kwa Afrika. Wakati Marekani ikiwa haijatosheka kunyonya utajiri mkubwa wa Afrika na rasilmali (zake), pia inatumia mbinu za kisiasa na kisheria kama hii ili kusahilisha njia ya sera zake za kigeni ikipatiliza udhaifu wa kimfumo wa bara la (Afrika)

Pia, kwa upande wa Urusi, maslahi yake ndani ya Afrika yanasukumwa na kitu kimoja tu, nacho ni unyonyaji wa kiuchumi, kwa kuwa nayo inakumbatia ubepari baada ya kuachana na ukomunisti, ikijihusisha kwa kiasi kikubwa na biashara kubwa ya silaha na vifaa vya kijeshi inayochukuwa zaidi ya asilimia 50 ya biashara zake barani Afrika. Maamiliano ya kibiashara baina ya Afrika na Urusi yalifikia dolari za kimarekani 17.4 billioni ndani ya mwaka 2017.


Marekani na ajenda yake ya kikoloni na ya kibepari haina kwa namna yoyote mamlaka ya kimaadili ya kulichagulia na kulilazimishia bara la Afrika rafiki au adui, bali inachohitaji Afrika ni mfumo wa kiuadilifu ambao ni wa Uislamu chini ya dola yake ya Khilafah, hapo (Afrika) itaweza kujikomboa na aina zote za idhilali za Marekani na za dola nyengine za kibepari.

**Masoud Msellem**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**
**Hizb ut Tahrir Tanzania**

 Email: info@uqab.or.ke

# HABARI NA MAONI
# Uislamu na Waislamu Wataendelea Kuteseka Bila kujali Nani Ameshinda au Ameshindwa kwenye Uchaguzi



**Habari:**

Wakenya mara kwa mara wanatazama mitandao ya kijamii na vyombo vya habari vya kawaida na kujaribu kutafakari ishara mchanganyiko kuhusu ni nani anayeweza kuwa Rais wao mpya. Naibu Rais William Ruto na kinara wa Upinzani Raila Odinga wanafuatana unyo unyo. (The Star, 13/8/2022).

**Maoni:**

Hivi sasa Kenya kama shamba la wakoloni inazama katika taharuki ya kisiasa kutokana na kuchelewa kutangazwa kwa mshindi wa urais. Mawakala wa kisiasa wanaowakilisha miungano shindani ya kisiasa wanatupiana tuhuma za wizi wa kura. Uhalisia juu ya uongozi wa Kenya yaani miundo ya kisiasa na kijeshi imefungwa minyororo na bwana mkoloni Uingereza. Kwa hivyo, sera zake za ndani na nje zinachorwa jijini London na kutekelezwa jijini Nairobi. Hivyo basi, uchaguzi ni mapambo tu ya kisiasa yanayotumiwa na bwana wa kikoloni kuwapa nguvu wasimamizi wa shamba lake.

Kwa hivyo, ni jambo la kushangaza kwa Waislamu kusherehekea kushinda au kushindwa kwa mgombea fulani haswa katika ngazi ya urais. Kwa kuwa, kuanzia mwanzo, chaguzi hizi za kidemokrasia ni haramu kwetu Waislamu kushiriki katika ngazi yoyote ile yaani kuanzia ngazi ya Wadi hadi Urais. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

﴿إِنِ ٱلۡحُكۡمُ إِلَّا لِلَّهِ﴾

"Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu" [Yusuf: 40]. Uharamu huu unatokana na ukweli kwamba tunachagua watu wa kwenda kutuwakilisha katika kutunga sheria na utawala kinyume na maamrisho ya Shari'ah ya Kiislamu.

Baya zaidi watawala hao mawakala wa kikoloni wanaapishwa kuwa maadui wa wazi wa Uislamu na Waislamu. Uadui wao unathibitishwa na sio tu matamshi yao bali na vitendo vyao. Wanapitisha na kutabikisha sheria na sera zilizoidhinishwa na wakoloni zinazolenga Uislamu na Waislamu kwa kisingizio cha kupiga vita misimamo mikali na ugaidi. Mfano mzuri ulikuwa mwaka wa 2008 wakati Raila Odinga - Waziri Mkuu wa wakati huo na William Ruto - wakati huo akiwa Waziri wa Kilimo na baadaye Elimu wote walikuwa sehemu ya serikali ya mseto iliyoongozwa na marehemu Rais Mwai Kibaki. Ilikuwa ni chini ya uongozi wao ambapo Sheria ya Kupambana na Ugaidi ilipitishwa na kuimarishwa zaidi katika miaka iliyofuata chini ya uangalizi wao.

Ripoti za hivi punde zinathibitisha kwamba kuna ongezeko la idadi ya Waislamu wanaohangaishwa na kukabiliwa na mauaji yaliyokiuka sheria. Isitoshe, wengine wanaangamizwa kiuchumi na vyombo vya usalama vya dola kufunga akaunti zao za fedha na utajiri wao kuekewa vikwazo! Baya zaidi kwa Waislamu, ni kuzinduliwa kwa makao makuu ya Kitengo cha Polisi wa Kupambana na Ugaidi (ATPU) jijini Mombasa mnamo tarehe 20 Julai 2022. Jumba hilo la kisasa la ATPU lenye thamani ya Sh81 milioni lilifadhiliwa na serikali ya kikoloni

*Endelea... UK 5*

ya Uingereza. Fauka ya hayo, Balozi wa Uingereza nchini Kenya, Jane Marriott, alisema Kenya ni mshirika mkuu wa usalama wa Uingereza katika Afrika Mashariki. Pia alisema ugaidi ni mojawapo ya matishio makubwa zaidi yanayoikabili Kenya na Uingereza, na kwa hivyo, ili kupambana na tishio hili, Uingereza itaendelea kufadhili juhudi za Kenya za kupambana na ugaidi kwa Sh1 bilioni kila mwaka! (The Star, 20/7/2022).

Inasikitisha kuona Waislamu wakijifanya mithili ya mbuzi wanaowakaribia 'mbwa mwitu' kuliwa, kwa jina la kuwasherehekea wanasiasa wa kidemokrasia ambao ndiyo sababu ya maisha yao mabaya. Kwa upande mwengine, kuufumbia macho muongozo wa Kiislamu, unaolingania kushikamana imara na Shari'ah ya Kiislamu yaani kutoridhika chini ya utawala wa Kikafiri unaoongozwa na Makafiri. Hakika, Waislamu wanaoishi katika tawala za kidemokrasia ni vipofu; ISIPOKUWA ikiwa wanafanya kazi usiku na mchana ili kuondoa hali halisi iliyopo na kuibadilisha kwa mfumo wa utawala wa Kiislamu, Khilafah itakayosimamishwa tena kwa njia ya Utume.

Khilafah ndio tumaini letu pekee la kweli, ngao na mlinzi wa Uislamu na Waislamu, mali yetu, damu yetu na heshima yetu. Kukosekana Khilafah kumetufanya sisi Waislamu kuwa mayatima, ambao kila mjinga anaweza kuwakejeli! Ni lazima tukumbuke kwamba matumaini yetu ya maisha ya amani na mafanikio katika dunia hii ya mapito na akhera yako katika Khilafah. Kwa hiyo, ni lazima tuwe sehemu ya Hizb ut-Tahrir na kuongeza juhudi zetu maradufu kama Umma Mmoja unaolingania Dola Moja inayoongozwa na Khalifah Mmoja. Utukufu wa ardhi zetu utaregeshwa na maadui wa Uislamu na Waislamu watapigwa vita na wamwagaji damu za Waislamu watalipizwa kisasi InshaAllah. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُخۡلِفُ ٱلۡمِيعَادَ﴾

**"Hakika Mwenyezi Mungu havunji miadi yake."**
[ Aali-Imran: 9].

Dunia nzima iko katika machafuko, kiongozi wa ulimwengu, Amerika anayeitwa kinara wa demokrasia inakaribia kuporomoka. Musichelewe kuchukua fursa hii nzuri ya kufanya kazi kwa ajili ya Khilafah ijayo.

Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya
Hizb ut Tahrir na

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# HABARI NA MAONI
# Washindi Na Watakaoshindwa Kwenye Uchaguzi Wa August Wote Ni Mawakala Wa Mfumo Uliofeli Wa Demokrasia

**Habari:**

Huku zikiwa zimesalia siku chache kabla ya kufanyika kwa uchaguzi wa Agosti 9, baadhi ya viongozi wa Kiislamu pamoja na Wanazuoni wa Serikali nchini, wamewataka Waislamu kuwafanyia tathmini na kuwahakiki wagombea wa viti tofauti ili kufanya maamuzi sahihi. Imekua ni hulka kwa wanavyuoni hawa kupindisha maana ya aya na kutumia vibaya kanuni za kifiqhi kama vile 'uovu mdogo' kuwataka Waislamu kushiriki kikamilifu katika uchaguzi.

**Maoni:**

Kutoa hukumu ya Kiislamu juu ya kushiriki kwenye chaguzi za Kidemokrasia kunatupasa kwanza kuangalia kwa kina  maana ya uchaguzi wa Kidemokrasia na hali hii itatubidi tuangalie kile kiitwacho uhalisia wa jambo (Tahqiq il Manat') i.e yaani ni uchaguzi na nini hasa maana ya Demokrasia kama mfumo wa kiutawala. Uchaguzi ni uwakilishaji ambapo mtu huchagua mtu amwakilishe kwenye kufanya jambo kwa niaba yake. Kinachofanya uchaguzi kuwa halali au haramu sio ule uchaguzi wenyewe kwa dhati yake bali ni kile kinachofungamana nao.

Neno la Demokrasia asili ni mkusanyiko wa matamshi mawili yenye asili ya Kigriki Demos ambao humaanisha watu na cratos ikimaanisha utawala kwa maana ni utawala wa watu. Utawala huu humaanisha wanadamu wanamiliki ubwana (sovereignity) unaowawajibisha watunge kanuni ambazo ndio hutukuzwa kuliko sheria za MwenyeziMungu swt. Hivyo Bunge au baraza la seneti, la wawakilishi au Congress zote katika demokrasia ni taasisi za kutunga kanuni. Sasa Demokrasia huchukua mbinu ya uchaguzi kila baada ya miaka 5 au 4 ya watu kuwachagua watu wawe ni wawakilishi wao katika kazi ya kutunga kanuni. Kwa kifupi chaguzi za Kidemokrasia zinafungika katika kitendo cha kutunga sheria ambacho kinagongana na Uislamu.

Kwa mujibu wa Uislamu, sheria sio miliki ya yoyote yule ila ni ya MwenyeziMungu swt. Yeye MwenyeziMungu swt  ndiye mteremshaji sheria hivyo sheria yoyote ile inayotungwa na mwanadamu haifai na ya kimakosa hatakama inaafikiana na ile ya MwenyeziMungu hii ni kwa kuwa kazi ya kuweka sheria si ya yoyote yule ila ni ya MwenyeziMungu swt. Bali Uislamu umewajibisha kufuata sheria za MwenyeziMungu swt.Asema Allah swt:



فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُواْ فِيٓ أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُواْ تَسْلِيمًا

**"Naapa na Mola Wako Mlezi hawawi na Imani ya kikamilifu hadi wakufanye wewe ni hakimu katika yale wanayozozana kisha isipatikani ndani ya vifua vyao uzito wowote katika yale uliyowahukumia na wajasilimishe kikamilifu"** [An-Nisai: 65]

Huu ndio uhalisia wa uchaguzi, hivyo kinachofanya uchaguzi uwe halali au sio halali sio uchaguzi wenyewe bali ni kazi inayofungamana nao. Kwa ujumla chaguzi za Kidemokrasia ni kinyume na sheria ya Kiislamu hivyo ni haramu kwa Waislamu kupigia debe na kuunga mkono vyama vya kisiasa vya Kidemokrasia na kushiriki kwa uchaguzi wake. Ni dhahir shahir kwamba kufanywa kwa chaguzi za kila mara za kidemokrasia ni jaribio la kuteka nyara hisia za mabadiliko kwa watu kwa mfumo uliofeli tayari. Washindi na wanaoshindwa kwenye chaguzi hizi za Kidemokrasia ni vibaraka wa mabeberu ambao kazi yao msingi ni kuziba aibu za Demokrasia zilizoitumbukiza Kenya na Afrika kwa ujumla kwenye maafa na mizozo.

Baya zaidi ni kuwaona wanavyuoni wa Serikali ambao baadhi yao wamekua ni wapambe wa wanasiasa wakipinda matumizi ya maana ya qaida madhara mepesi wakiwataka Waislamu wasijifunge na sheria za Kiislamu na kufanya kazi ya kuleta mabadiliko ya kweli, yaani kuulingania Uislamu uweze kutawala dunia chini ya Khilafah  Raashida kwa mfumo wa unabii. Kiini cha majanga yanayokabili Kenya sio nani anatawala bali ni anatawalisha kwetu mfumo gani. Maadamu nchi inaendelea kutawaliwa na kanuni na tungo za Kidemokrasia tofauti na sheria za alizoteremsha MwenyeziMungu basi hatutoona mabadiliko ya kikweli.

**Imeandikwa kwa Niaba ya Ofisi kuu ya Habari ya Hizb ut-Tahrir na**

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**



# Je, Haiba ya Kimataifa Inapatikana kupitia Kuwatumikia Maadui wa Uislamu?

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Abu Ibrahim Bilal**

Shirika la Anadolu katika makala, "Mamlaka ya Uturuki katika uwanja wa kimataifa yanaongezeka," linatoa mukhtasari wa hotuba ya Rais wa Uturuki Erdogan kwa wawakilishi wa chama tawala cha Haki na Maendeleo.

"Katika miaka ya hivi karibuni, mamlaka ya Uturuki katika uwanja wa kimataifa yamekuwa yakiongezeka kwa kasi. Hayo yamesemwa na Rais Recep Tayyip Erdogan katika mkutano na wawakilishi wa chama tawala cha Haki na Maendeleo jijini Ankara.

Kulingana na rais huyo wa nchi, Uturuki ya leo inatetea kwa uthabiti maslahi yake ya kitaifa kwenye majukwaa yote, ikiwemo UN na NATO.

Kiongozi huyo wa Uturuki alibainisha kuwa nchi hiyo inafanikiwa kufikia matokeo yaliyokusudiwa, huku ikitekeleza diplomasia yenye ufanisi.

Rais Erdogan pia aliongeza kuwa kutokana na sera zinazofuatwa na mamlaka katika miongo miwili iliyopita, Uturuki imekuwa "nchi ya kidemokrasia zaidi na huru, nchi yenye fursa sawa." Chanzo: (Shirila la Anadolu)

Bila shaka, dori ya Uturuki katika kutatua matatizo mengi ya kieneo na kimataifa imeongezeka sana. Hii inaonekana kupitia ushiriki changamfu wa Uturuki katika matukio ya Syria, Libya, Nagorno-Karabakh, Afghanistan, Ukraine na maeneo mengine. Lakini, ushiriki huu ufungwa na dori ya mpatanishi na mtekelezaji pekee, lakini sio kama mtu mwenye kuamua mkakati na kufanya uamuzi.

Je, ni ukuaji upi wa haiba ya Uturuki katika uwanja wa kimataifa anaozungumzia Erdogan, ambaye sera yake ndani ya Uturuki yenyewe imegeuka kuwa mgogoro mwingine mkali? Makadirio ya Chama cha Haki na Maendeleo kinachoongozwa na Erdogan yalishuka hadi kiwango cha chini kiasi kwamba kikalazimika kuunda muungano wa wabunge kwa jina Muungano wa Watu, kikiunganishwa na Harakati ya Kitaifa ya mrengo wa kulia. Na wakati huo huo, alitangaza baadhi ya harakati za Kiislamu kuwa ni zenye misimamo mikali na za kigaidi na kuanza kuwatesa kikatili, hata wale ambao alipitia mabegani mwao kuingia madarakani.

Mtu yeyote na asishangazwe na maneno ya Erdogan, ambaye, kwa kukurupuka kiujinga, anakadiria, labda, kuwa ndio tumaini la pekee la ulimwengu wa Kiislamu, kwamba wakati wa utawala wake Uturuki imekuwa nchi ya kidemokrasia zaidi. Yote tisa, kumi Uturuki ya kisasa ni jamhuri ya kisekula iliyoundwa juu ya magofu ya Khilafah ya Kiuthmani, iliyovunjwa na mikono ya kibaraka wa Uingereza Mustafa Kemal. Na Erdogan, aliyeingia madarakani chini ya pazia la "mwanasiasa wa Kiislamu na mwanamageuzi", kupitia kukiri kwake mwenyewe, ni mlezi mwaminifu wa vima na maadili ya jamhuri, ambayo ni usekula na utaifa wa Kituruki.

*Endelea... UK 8*

Tangu kuanzishwa kwake hadi leo, sera ya serikali tawala ya Uturuki, pamoja na nchi nyingine za Kiislamu, ambazo mipaka yake, katiba na muundo wao wa kisiasa huamuliwa na wakoloni wa Magharibi, zina majukumu mawili pekee.

Kwanza, kuzuia maendeleo ya Umma wa Kiislamu na kuregea kwake katika mfumo kamili wa maisha ya Kiislamu, kwa kupotosha na kubadilisha imani na hisia zake za Kiislamu kwa fikra za usekula, uzalendo, utaifa nk.

Jambo la pili ni kutumikia kwa utiifu maslahi ya dola kuu za kirasilimali katika mapambano yao ya ushindani wa kuitawala dunia, kutumia mali na maisha ya Waislamu kama bidhaa ya bei nafuu.

Erdogan bila aibu anajigamba ushiriki wa Uturuki katika shughuli za miundo ya kisiasa inayochukia Uislamu, ikiwemo Umoja wa Mataifa na NATO, akiitaja kuwa ni ulinzi wa maslahi ya taifa. Wakati mashirika haya si chochote zaidi ya zana za kuhifadhi utawala wa mfumo wa kirasilimali katika uwanja wa kimataifa, ukiongozwa na Marekani, iliyoketi kileleni mwa siasa za dunia kufuatia matokeo ya Vita vya Pili vya Dunia. Linapokuja suala la kulinda dini, heshima na maisha ya Waislamu, Erdogan anajifunga tu na kumwaga machozi hadharani na kauli tupu zinazotikisa upepo.

Utawala wa Uturuki, ukiongozwa na Erdogan, umecheza dori muhimu katika kuyanyonga mapinduzi ya Waislamu wa Syria dhidi ya udikteta katili wa kibaraka wa Marekani Assad, kuwashawishi na kuwahonga makamanda wengi wa waasi kwa fedha na ahadi za uongo kwenye meza makongamano tofauti tofauti ya "marafiki wa Syria", nk. Chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa, kando na jeshi la ISAF la Uturuki kushiriki katika uvamizi na miaka ishirini ya kuikalia Afghanistan. Uturuki pia inaendelea kupigia debe uhamisho wa ushawishi wa Ulaya katika koloni za zamani za Afrika na ushawishi wa Urusi katika dola za zama za baada ya Usovieti za Caucasus na Asia ya Kati kwa niaba ya Marekani.

Uturuki haikusimama kando wakati wa uvamizi wa sasa wa Urusi dhidi ya Ukraine, ambayo ilitumika kama sababu ya kuanzishwa kwa vikwazo vikali dhidi ya Urusi ambavyo viligonga kwa uchungu maslahi ya kiuchumi ya nchi za EU, ambazo zinategemea sana usambazaji wa rasilimali za nishati za Urusi. Ikiuza aina za kisasa za silaha kwa Kyiv, Ankara wakati huo huo inaendelea na ushirikiano wa karibu na Moscow, ikiwemo kununua kutoka kwake mifumo ya kisasa ya ulinzi wa anga yenye thamani ya mabilioni ya dolari za Marekani.

Hotuba ya Erdogan inashuhudia kwamba yeye, mithili ya vibaraka wengine walioketishwa na wakoloni wa Kimagharibi juu ya shingo za Umma wa Kiislamu, anapima mafanikio kwa kiwango cha usaliti wa maslahi ya Uislamu na Waislamu kwa ajili ya kutumikia maslahi ya maadui wa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, mtu yeyote na asihadaike na uchaji Mungu wa kujifanyisha na hotuba za uwongo za madhalimu waovu walionyakua utawala. Yote tisa, kumi hili halitageuka kuwa chochote kwao, isipokuwa fedheha na adhabu kali itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

بَشِّرِ ٱلْمُنَٰفِقِينَ بِأَنَّ لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا * ٱلَّذِينَ يَتَّخِذُونَ ٱلْكَٰفِرِينَ أَوْلِيَآءَ مِن دُونِ ٱلْمُؤْمِنِينَ أَيَبْتَغُونَ عِندَهُمُ ٱلْعِزَّةَ فَإِنَّ ٱلْعِزَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا

**“Wabashirie wanaafiki kwamba watapata adhabu chungu, Wale ambao huwafanya makafiri kuwa ndio marafiki badala ya Waumini. Je! Wanataka wapate kwao utukufu? Basi hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu.”** [4:138-139].

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliuita Umma wa Muhammad (saw) kuwa ni umma bora uliopo kwa manufaa ya wanadamu wote, akataja kabla ya kumuamini Yeye, wajibu wa Waislamu kuamrisha mema na kujiepusha na yale yaliyoharamishwa. Kutokana na Sunnah ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) na makhalifa waongofu (ra) inajulikana kuwa njia ya kufanya hivyo ni kuwaunganisha Waislamu chini ya uongozi wa Khalifa mmoja, anayetabikisha sharia, katika sera ya ndani ya dola pamoja na katika kiwango cha mahusiano ya kimataifa.

Kwa kuwa kuwepo kwa jamii katika Uislamu hakupimwi na uchamungu wa watu binafsi kipeke yao na wingi wao, bali kwa ubwana wa ada na kanuni za Sharia ndani yake.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ

**“Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu.”** [3:110].

Mamlaka ya kimataifa bila shaka yataregea kwa Umma wa Kiislamu kwa kuregeshwa kwa dola moja ya Kiislamu katika muundo wa Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya utume. Kupitia kuugeuza Uislamu kuwa mfumo wa kisiasa, Umma wa Kiislamu utaregea katika uga wa kimataifa kama raia kamili na nguvu yenye ushawishi mkubwa yenye uwezo wa sio tu kulinda maslahi yake, bali pia kuonyesha njia ya wokovu na maendeleo kwa wanadamu wote. Na itakuwaje vyenginevyo, kwa sababu nguvu na ushawishi wake utatokana na uongozi wa Mola Mlezi wa mbingu na ardhi Mwenye Nguvu na Mwenye hekima, na sio kutokana na maazimio ovyo na maovu ya pote la wanafiki na wapagani. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَجَعَلَ كَلِمَةَ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ ٱلسُّفْلَىٰ وَكَلِمَةُ ٱللَّهِ هِىَ ٱلْعُلْيَا وَٱللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

**“na akalifanya neno la walio kufuru kuwa chini, na Neno la Mwenyezi Mungu kuwa ndilo juu. Na**

*Endelea... UK 9*



Email: info@uqab.or.ke

**Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu Mwenye hikima.”** [9:40].

Uadilifu wa mfumo wa kisiasa na kiuchumi wa Kiislamu, unaotabikishwa na Khilafah, utaurudisha Umma wa Kiislamu kwenye nguvu zake za zamani. Kama ilivyokuwa hapo awali, neno moja kutoka kwa Khalifa litatosha kukomesha mashambulizi yoyote dhidi ya Waislamu na maadili yao kutoka kwa makafiri. Majeshi ya Mujahidina yatakomboa ardhi za Kiislamu na kuangamiza vizuizi vya vyama vya kitaifa na kieneo vilivyoanzishwa na wakoloni. Wakiungana ndani ya dola moja, chini ya bendera za LA ILAHA ILLA ALLAH MUHAMMAD RASULULLAH, Waislamu wataeneza nuru ya Uislamu kwa watu kote duniani, wakiulingania kupitia diplomasia na jihad yenye ufanisi.

**هُوَ ٱلَّذِى أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِٱلْهُدَى وَدِينِ ٱلْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى ٱلدِّينِ كُلِّهِ وَكَفَى بِٱللَّهِ شَهِيدًا**

**“Yeye ndiye aliye mtuma Mtume wake kwa uwongofu na Dini ya Haki, ili aitukuze juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi.”** [48:28]



**Email: info@uqab.or.ke**

**JIBU LA SWALI**

# Swadaqa Ya Mwana Mwema Kumtolea Mzazi Wake Aliyekufa, Thawabu Zitamfikia?



**Swali:**

Assalamu Alaikum Wa Rahmatullahi Wa Barakatuh! Maamkuzi kwenu ewe sheikh wetu na amiri wetu, kutoka nyoyoni mwetu.

Amesema Mtume (saw):

«إذا مات ابن آدم انقطع عمله إلا من ثلاث، صدقة جارية، علم ينتفع به، أو ولد صالح يدعو له»

**“Pindi mwanaadamu anapokufa basi (thawabu za) matendo yake hukatika, isipokuwa kutokana na mambo matatu: swadaqa yenye kuendelea, elimu ambayo watu wananufaika nayo, au mtoto mwema anayemuombea dua”.**

Je, sadaqa inayoendelea ni sharti iwe ni ile ambayo maiti alikuwa ameitoa kabla ya kufa kwake? Ama hata watoto wake wakiitolea roho yake pia itahisabika?

Mwenyezi Mungu aziweke sawa hatua zenu juu ya haki, na awashike mikono kufikia yenye izza kwa Ummah.

**Jibu:**

Wa Alaikum Salaam Wa Rahmatullahi Wa Barakaatuh.

Hadith hiyo ni kuhusu matendo ya maiti “matendo yake hukatika, isipokuwa kutokana na mambo matatu” nayo ni: swadaqa inayoendelea, na elimu yenye manufaa, au mwana mwema anayemuombea”

Ama kuhusu matendo ya wengine kumfikia maiti: kuna matendo ambayo wengine wakiyafanya kwa niaba yake thawabu humfikia, na miongoni mwayo ni swadaqa ambayo watoto wake watamtolea, na wakakusudia thawabu zake zimfikie yeye:

1- Amesema Shawkani katika Nail ul-Autwaar:

[Na imepokewa kutoka kwa Abu Huraira kwamba,

أَنَّ رَجُلاً قَالَ لِلنَّبِيِّ ﷺ: إِنَّ أَبِي مَاتَ وَلَمْ يُوصِ، أَفَيَنْفَعُهُ أَنْ أَتَصَدَّقَ عَنْهُ؟ قَالَ:« نَعَمْ»

*Endelea... UK 11*



Email: info@uqab.or.ke

“Mwanaume mmoja alimwambia Mtume (saw) hakika babangu amekufa na hakutoa wasiya, je kutamnufaisha mimi kumtolea swadaqa? Akasema: “**ndio**” (imepokewa na Ahmad, Muslim, Nasaai, na Ibn Maajah).

Na kutoka kwa Aisha, kwamba

**أَنَّ رَجُلاً قَالَ لِلنَّبِيِّ ﷺ: إنَّ أُمِّي اُفْتُلِتَتْ نَفْسُهَا، وَأُرَاهَا لَوْ تَكَلَّمَتْ تَصَدَّقَتْ، فَهَلْ لَهَا أَجْرٌ إنْ تَصَدَّقْتُ عَنْهَا؟ قَالَ نَعَمْ**

“Mwanaume mmoja alimwambia Mtume (saw) hakika mamangu amekufa ghafla, na nadhani lau angezungumza basi angetoa swadaqah, je atakuwa na malipo ikiwa nitamtolea swadaqah? Akasema: “**ndio**” (Bukahri na Muslim)

Na kutoka kwa Hasan,

**عَنْ سَعْدِ بْنِ عُبَادَةَ أَنَّ أُمَّهُ مَاتَتْ فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، إنَّ أُمِّي مَاتَتْ أَفَأَتَصَدَّقُ عَنْهَا؟ قَالَ: نَعَمْ قُلْتُ: فَأَيُّ الصَّدَقَةِ أَفْضَلُ؟ قَالَ: سَقْيُ الْمَاءِ**

“Kutoka kwa Saad bin Ubaada, kwamba mamake alikufa, akasema (Saad): “Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hakika mamangu amekufa, je, nimtolee swadaqah?” Akasema: “**ndio**” nikasema: ni ipi swadaqah bora zaidi? Akajibu: “**ni kunywesha maji**”. Akasema Hasan: huo ndio unyweshaji wa watu wa Saad huko Madina. (imepokewa na Ahmad na Nasaai).

(Mlango wa Thawabu za Jamaa wa Karibu Kuwazawadia Wafu)

Neno lake (hilo litamnufaisha): ndani yake kuna dalili kwamba, mwana anachomfanyia babake Muislamu – kama vile saumu, na swadaqah – thawabu zake humfikia (babake)

… neno lake (ni kunywesha maji): ndani yake kuna dalili ya kwamba, kunywesha maji ndio swadaqah bora zaidi.

Na katika mapokezi ya Abu Dawud:

**“فَأَيُّ الصَّدَقَةِ أَفْضَلُ؟ قَالَ: الْمَاءُ، فَحَفَرَ بِئْراً وَقَالَ: هَذِهِ لِأُمِّ سَعْدٍ“**

**“Basi ni swadaqah gani bora zaidi?”** Akajibu: “**Ni maji, basi akachimba kisima, na akasema: hiki kitakuwa kwa ajili ya mamake Saad**”.

Na hadith hii imepokewa pia na Daaraqutni kwenye Gharaib ya Malik. Na imepokewa katika Al-Muatwa kwa hadith ya Said bin Saad bin Ubaada kwamba Saad alitoka pamoja na Mtume (saw) kwenye baadhi ya vita vyake, na mamake (Saad) akafikwa na mauti huko Madina, akaambiwa: acha wasiya, akasema: nitatoaje wasiya na mali ni za Saad! Akafa kabla ya Saad kurudi…” Akaitaja hadith (kwa ukamilifu).

Na kumesemwa: yule mwanaume ambaye hakutajwa jina katika hadith ya Bi Aisha na katika hadith ya Ibn Abbas ni Saad bin Ubaada. Na kinachojulisha hilo ni kwamba, Bukhari baada ya hadith ya Aisha ameleta hadith ya Ibn Abbas kwa tamshi: “Hakika Saad bin Ubaada alisema: hakika mamangu amekufa akiwa na nadhiri” na ni kama ameashiria kuwa ambaye hakutajwa jina kwenye ile hadith ya Aisha ni Saad. Hadithi za mlango huu zajulisha kwamba (thawabu) za swadaqa ya mtoto humfikia wazazi wawili baada ya kufa kwao, hata bila ya wao kuacha wasiya. Hivyo, kwa hadith hizi hufanyiwa takhsisi ujumla wa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**﴿وَأَنْ لَيْسَ لِلإِنْسَانِ إِلا مَا سَعَى﴾**

**“Na ya kwamba hatapata mtu ila aliyo yafanya mwenyewe?”** [An-Najm: 39].

Lakini hakuna katika hadith za mlango huu zaidi ya kwamba swadaqa kutoka kwa mtoto humfikia mzazi, na bila shaka imethubutu kwamba mtoto ni katika matendo yake, kwa hiyo hakuna haja ya kudai takhsisi…].

2- Sherhe ya An-Nawawi juu ya Sahih Muslim:

[…kutoka kwa Aisha,

**أَنَّ رَجُلاً أَتَى النَّبِيَّ ﷺ فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، إِنَّ أُمِّيَ افْتُلِتَتْ نَفْسَهَا وَلَمْ تُوصِ وَأَظُنُّهَا لَوْ تَكَلَّمَتْ تَصَدَّقَتْ أَفَلَهَا أَجْرٌ إِنْ تَصَدَّقْتُ عَنْهَا؟ قَالَ: نَعَمْ.**

“Kwamba mwanaume mmoja alikuja kwa Mtume (saw) akamwambia: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika mamangu amekufa ghafla, na hakuacha wasiya. Na nadhani lau angeongea basi angelitoa swadaqa, hivi je, atakuwa na malipo ikiwa nitamtolea swadaqa? Akajibu: “**ndio**” …

Na katika hadith hii: swadaqah anayotolewa maiti humnufaisha, na thawabu zake humfikia maiti, na hilo ni kwa makubaliano ya wanazuoni. Na pia wamekubaliana kwamba dua humfikia, na ulipaji deni, kwa mujibu wa nususi zilokuja kuhusiana na hayo yote. Na kumfanyia hajj maiti yasihi ikiwa ni hijjah ya Uislamu (ya faradhi), na hivyo hivyo kama atakuwa ameacha wasiya wa kufanyiwa hijjah ya ziyada (Sunnah) katika kauli sahihi zaidi kwetu (shaafiiyah) na wametafautiana wanazuoni kuhusu la sawa ikiwa mtu atakufa hali anadaiwa saumu, ila kauli yenye nguvu ni kuwa yaruhusiwa kumfungia, kutokana na hadithi nyingi sahihi katika hilo. Na kauli mashuhuri katika madhehebu yetu ni kwamba thawabu za kusoma Qur`an hazimfikii maiti, na kundi katika watu wetu wamesema thawabu zamfikia, na huo ndio msimamo wa Ahmad bin Hanbal. Ama kuhusu swala na ibada zengine: thawabu zake hazimfikii, (huo ndio msimamo) wetu na wa wanazuoni wengi, na Ahmad amesema: thawabu zote zamfikia kama ilivyo (thawabu) za hajj].

Hivyo basi, wewe kumtolea mzazi wako swadaqah na ukamkusudia, thawabu zake zitamfikia Mwenyezi Mungu akipenda.

***Endelea... UK 12***

 **Email: info@uqab.or.ke**

Na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi na Mwenye hekima zaidi.

**Ndugu Yenu**

**Ataa Bin Khalil Abu Rashtah**

**9 Ramadhan 1443 H**

**10/4/2022 M**

